Taarifa kwa vyombo vya habari|Kutolewa hivi karibuni

# Matokeo ya kujifunza kitaifa bado ni duni. Watoto 3 tu kati ya 10 wa darasa la 3 ndio uwezo wa kufaulu mtihani wa darasa la 2

Wilaya ya Mbeya mjini inoongoza kwa ufaulu. Watoto 3 kati ya 4 (wenye miaka 9-13) wa wilaya hiyo wana uwezo stahiki wa kusoma na kuhesabu

**Dar es Salaam, Julai 29, 2015:** Licha ya matarijio kuwa watoto wote wa darasa la 3 wangeweza kusoma Kiswahili na Kiingereza, pamoja na kufanya hesabu rahisi za darasa la pili, ripoti mpya ya utafiti inaonesha kuwa ni wanafunzi wachache mno wenye uwezo huo.

**Kiswahili**

- Nusu ya watoto wa darasa la 3 (45%) wanaweza kusoma hadithi ya Kiswahili ya kiwango cha darasa la 2.
- Waliofika darasa la 7, ni 4 kati ya 5 (80%) wenye uwezo wa kusoma Kiswahili cha darasa la 2. Hii inaashiria kuwa 20% ya wanafunzi humaliza darasa la 7 wakuwa hawawezi kusoma Kiswahili.

**Kiingereza**

- Wanafunzi 2 kati ya 10 (19%) wa darasa la 3 wanaweza kusoma hadithi ya Kiingereza ya darasa la 2.
- Waliofika darasa la 7, ni watoto 6 kati ya 10 (56%) wenye uwezo wa kusoma hadithi ya Kiingereza ya kiwango cha darasa la 2. Takriban nusu ya wanafunzi wote wa darasa la 7 hawajui kusoma Kiingereza, lugha ya kufundishia shule za sekondari.

**Hesabu**

- Watoto 3 kati ya 10 wa darasa la 3 (31%) wanaweza kufanya kwa usahihi hesabu ya kuzidisha za darasa la 2.
- Watoto 3 kati ya 10 (29%) wa darasa la 7 hawawezi kufanya hesabu za kuzidisha za darasa la 2.

Matokeo haya yametolewa leo na Uwezo iliyopo Twaweza katika uzinduzi wa ripoti ya utafiti iitwayo *Je, Watoto wetu wanajifunza? Uwezo wa Kusoma na kuhesabu nchini Tanzania 2014.* Ripoti hii ni ya nne tangu mwanzo wa tathmini hizi za kila mwaka. Utafiti huu ulifanyika mwaka 2013. Washirika wa Uwezo waliwapima watoto 100,000, wenye umri wa miaka 7-16, kwenye wilaya 131 katika mikoa 25.

Tofauti za kiuchumi na kijiografia zinaaendelea kuathiri uwezo wa watoto kujifunza.

*Ukiangalia kijiografia watoto wa miaka 7 hadi 16, kuna tofauti ya ufaulu wa takribani 20% kati ya watoto wa maeneo ya vijijini na wale wa mjini kwenye masomo yote matatu.*

- Ni 67% ya watoto wa mjini wanaoweza kusoma hadithi ya Kiswahili cha darasa la 2, ukilinganisha na 46% tu ya wenzao wa vijijini.
- Ni 44% ya watoto wa mjini wanaoweza kusoma hadithi ya Kiingereza cha darasa la 2, ukilinganisha na 26% tu ya wenzao wa vijijini.
- Ni 54% ya watoto wa mjini wanaoweza kufanya hesabu rahisi za kuzidisha za darasa la 2, ukilinganisha na 36% tu ya wenzao wa vijijini.

| Nafasi | Wilaya | % | Nafasi | Wilaya | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mbeya (mjini) | 74% | 127 | Tunduru | 23% |
| 2 | Bukoba (mjini) | 71% | 128 | Uyui | 23% |
| 3 | Iringa (mjini) | 70% | 129 | Musoma (vijijini) | 22% |
| 4 | Arusha (mjini) | 69% | 130 | Nkasi | 20% |
| 5 | Morogoro (mjini) | 67% | 131 | Masasi | 19% |

*Asilimia ya watoto wenye miaka 9-13 ambao walifaulu majaribio ya masomo yote matatu, kwa nafasi kiwilaya (wilaya tano za ufaulu wa juu na tano za chini), mwaka 2013.*

*Wilaya zote zenye ufaulu wa juu ni za mijini. Na zile zenye ufaulu duni ni za vijijini.*

*Kuna tofauti kubwa ya uwezo wa kusoma na kuhesabu kati ya watoo tajiri na maskini.*

- Ni 57% ya watoto tajiri wanaoweza kusoma hadithi ya Kiswahili cha darasa la 2, ukilinganisha na 40% tu ya watoto maskini.
- Ni 35% ya watoto tajiri wanaoweza kusoma hadithi ya Kiingereza cha darasa la 2, ukilinganisha na 20% tu ya watoto maskini.
- Ni 46% ya watoto tajiri wanaoweza kufanya hesabu rahisi za kuzidisha za darasa la 2, ukilinganisha na 31% tu ya watoto maskini.

Pamoja na tofauti hizi, takwimu zinaonesha kuwa watoto wenye wazazi wasomi wana matokeo bora zaidi ya kujifunza. Watoto 3 kati ya 4 (73%) wenye wazazi waliomaliza elimu ya sekondari waliweza kusoma hadithi ya Kiswahili. Lakini ni nusu tu (48%) ya watoto ambao wazazi wao hawakusoma ndio walioweza kusoma hadithi ya Kiswahili.

Hata hivyo, kuna habari nzuri kuhusu suala la usawa wa jinsia. Hakukuonekana tofauti yoyote ya ufaulu kati ya wavulana na wasichana kwenye kusoma Kiswahili, Kiingereza au kuhesabu. Vile vile hakukuwa na tofauti za kijinsia kwenye suala la mahudhurio. Ingawa matokeo ya kujifunza yako chini, hali hii haibagui wasichana wala wavulana.

Uwezo ilikusanya takwimu nyingi kuhusu ubora wa vifaa vya shule.

- Asilimia 44 ya shule zinatoa chakula kwa wanafunzi
- Asilimia 46 ya shule zinapata maji ya kunywa safi na salama
- Asilimia 31 ya shule zina maktaba
- Kwa wastani wanafunzi 30 wanatumia kitabu cha kiada kimoja, na kila darasa lina wanafunzi 74.

*Ingawa matokeo ya Uwezo yamekuwa yakionesha na yanaendelea kuonyesha viwango duni vya kujifunza kwa miaka kadhaa, kuna tofauti kubwa miongoni mwa watoto. Watoto wanaotoka familia maskini bado wamebaki nyuma,* "Alisema Zaida Mgalla, Meneja wa Uwezo Tanzania. *"Lakini kuondoa tofauti za kijinsia katika suala la upatikanaji wa elimu ni mafanikio ambayo yanaonesha kuwa juhudi za pamoja kimataifa na kitaifa zinaweza kuleta mabadiliko."*

Aidan Eyakuze, Mkurugenzi Mtendaji wa Twaweza alisema *"takwimu zinaendelea kuonesha tatizo kubwa lililopo kwenye mfumo wetu wa elimu. Watoto hawapati stadi za msingi za elimu ya msingi. Lakini si shule zote ama wanafunzi wote wanaolingana katika kutokufaulu. Kwenye mifano ya mafanikio mazuri, tunaweza kupata mawazo mazuri, msukumo chanya na mbinu bora za kuhakikisha watoto wetu wote wanajifunza wakiwa shuleni.''*

Tathmini ya kujifunza ya Uwezo hufanywa nchini Kenya, Tanzania na Uganda na maelfu ya wananchi waliojitolea. Watoto wenye umri wa miaka 6 hadi 16 hupimwa ujuzi wa kusoma na kuhesabu kwa

kutumia majaribio ya mtaala wa darasa la 2. Uwezo inalenga kuweka mijadala ya kitaifa kuhusu elimu, matokeo ya kujifunza na vipaumbele vya sera.

**---Mwisho---**

**Kwa taarifa zaidi:**


Tunu Yongolo
**Baruapepe:** tyongolo@twaweza.org

Fausta Musokwa
Baruapepe: ms_fausta@yahoo.co.uk


**Maelezo kwa Wahariri**

- Ripoti nzima, pamoja na mifano ya majaribio yaliyotumika vinapatikana www.uwezo.net **Kuhusu Twaweza**
- Twaweza inafanya kazi kuwezesha watoto kujifunza, wananchi kuwa na utayari wa kuleta mabadiliko na serikali kuwa wazi zaidi na sikivu katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda. Tuna programu, wafanyakazi na ofisi katika nchi zote tatu, na utaratibu unaoheshimika kimataifa wa kujifunza, ufuatiliaji na tathmini. Programu zetu muhimu ni pamoja na *Uwezo*, tathmini kubwa ya kila mwaka ya wananchi barani Afrika inayopima viwango vya watoto vya kujifunza kwenye maelfu ya kaya, na *Sauti za Wananchi*, utafiti wa kwanza Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaofanyika kwa njia ya simu ya mkononi. Pia tunashiriki kwenye masuala ya umma na sera, kupitia ubia wetu na vyombo vya habari, juhudi za kimataifa zinazoshughulikia masuala ya uongozi kama vile mpango wa Ushirikiano na Serikali wazi (OGP).